## HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA ULINZI WA MWANAMKE NA MTOTO WILAYA KILICHOFANYIKA TAREHE 26/09/2018 KWENYE UKUMBI WA IDARA YA MAJI

**WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | KHAMLO M. NJOVU | Ag. DED | MWENYEKITI |
| 2. | BARAKA MSUYA | Ag. DCDO | KATIBU |
| 3. | MAGRETH EGBERT LYARO | DAWATI (P) | MJUMBE |
| 4. | NORBERT D. NTACHO | | MJUMBE |
| 5. | SUZANA R. MHEKELA | | MJUMBE |
| 6. | ADRIAN J. MPAGAMA | MASHUHURI | MJUMBE |
| 7. | VERDIANA D. NYANG'OLO | VIKUNDI | MJUMBE |
| 8. | HONORATA M. KABUNDUGURU | DEO SEKONDARI | MJUMBE |
| 9. | KANDIDO M. MNEMELE | W. ULEMAVU | MJUMBE |
| 10. | REUBEN J. MWATWINZA | A.UTAMADUNI | MJUMBE |
| 11. | ROMAN MTONO | UHAMIAJI | MJUMBE |
| 12. | SABAH MOHAMED SEIF | SHEKH | MJUMBE |
| 13. | DEBORA M. MNYANG'ALI | RMPC (Mh. Hakimu) | MJUMBE |
| 14. | VAILETH M. NOLASCO | MASHUHURI | MJUMBE |
| 15. | SHAIBU J. MASASI | TEHAMA | MJUMBE |
| 16. | ANTHONY N. MBABILE | DSWO | MJUMBE |
| 17. | MARY CHAKUPEWA | DEO (M) | MJUMBE |
| 18. | HAPPINESS E. NUSU | MCHUMI | MJUMBE |
| 19. | GLADYS UDOBA | VIKUNDI | MJUMBE |
| 20. | ISAYA R. MGWAZI | AZISE | MJUMBE |
| 21. | JOSEPH JACKSON M | Kny: MWANASHERIA | MJUMBE |
| 22. | KIBIBI EDWARD | HRO | MJUMBE |
| 23. | RENATUS KOMBA | AFISA LISHE | MJUMBE |
| 24. | DR. SAID MAWJI | DMO | MJUMBE |
| 25. | GODFREY AYAKO | DLFO | MJUMBE |
| 26. | BILTON T. OTTO | DTO | MJUMBE |

**WASIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | PADRI DAVID NGIMBA | - | Bila Taarifa |

**WAALIKWA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | EVANCE ANTHON | CDF | MUALIKWA |
| 2. | GODWIN CHILOMO | CDF | MUALIKWA |
| 3. | CLARA WISIKO | CDF | MUALIKWA |
| 4. | ASHA RAMADHANI | CDF | MUALIKWA |
| 5. | FADHILI MOLLEL | SWO | SEKRETARIET |
| 6. | BERNADETH KAMUGISHA | CDO | SEKRETARIET |
| 7. | MPANGALA I. MAGNUS | PCDO | SEKRETARIET |

**AGENDA**

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda za Kikao
3. Taarifa ya Uundwaji wa Kamati za Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto za Kata na Taarifa ya Mabaraza ya Watoto ya Kata.
4. Taarifa ya Wadau Juu ya Ulinzi wa Mtoto (CDF na TAYOA)
5. Kuandaa Mpango Kazi wa Kamati Robo ya pili
6. Mengineyo kwa Ruhusa ya Mwenyekiti
7. Kufunga Kikao

**Agenda. Na 1:01:2018/2019: Kufungua Kikao**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 10:36 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha kwanza kwa Mwaka wa Serikali wa 2018/2019. Mwenyekiti alitoa maelezo kwenye kikao hiki cha kwanza wajumbe watapata fursa ya kujua kuwa nini tunafanya, kazi zilizofanyika kwa kipindi cha robo mwaka Julai – Septemba 2018 na Mipango ya baadae, hivyo aliwaomba wajumbe michango yao katika kikao ili kuweza kufikia Malengo ya kumlinda Mwanamke na Mtoto.

**Agenda. Na 2:01:2018/2019: Kuthibitisha Agenda za Kikao**

Katibu alisoma Agenda za kikao ambazo zilikuwa agenda nane, ambazo ni Kufungua kikao, Kuthibitisha Agenda, za kikao, Taarifa ya Kamati ya Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto ya Kata, na Taarifa ya Mabaraza ya Watoto ya Kata, Taarifa ya Wadau Juu ya Ulinzi wa Mtoto (CDF na TAYOA), Kuandaa Mpango kazi wa kamati robo ya Pili, Mengineyo kwa Ruhusa ya Mwenyekiti, na Kufunga Kikao. wajumbe kwa pamoja walipitia agenda hizo na kukubaliana kuwa ndio zitakuwa agenda za kikao hiki.

Kabla ya Agenda nyingine kuendelea Mratibu wa Mradi wa Utu wa Mtoto aliomba ridhaa ya wajumbe kupigwa picha zao wakati kikao kinaendelea. Aidha, alifafanua kuwa picha hizi ni kwa ajili ya matumizi ya Ofisi na kuweka kumbukumbu na utoaji wa Taarifa na siyo vinginevyo. Wajumbe kwa pamoja waliridhia kwa kujaza fomu maalum ya ridhaa na kuweka saini zao.

**Agenda. Na 3:01:2018/2019: Taarifa ya Uundwaji wa Kamati za Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto za Kata na Taarifa ya Mabaraza ya Watoto ya Kata.**

Taarifa ya Uundwaji wa Mabaraza ya Watoto na Kamati ya Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto kwa kuangalia Kata ambazo zina Mabaraza ya Watoto na Kamati ya Ulinzi ya Mwanamke na Mtoto ngazi ya Kata. Wajumbe walihoji kuwa taarifa inaonyesha baada ya Wiki mbili shughuli iwe imekamilika lakini taarifa haijaonyesha ni lini ufafanuzi ulitolewa ni kwa muda gani wiki mbili zitakuwa zimekwisha?

Majibu kutoka kwenye Sekretarieti muda wa Wiki mbili ni kuanzia tarehe 27/09/2018. Wajumbe walishauri kuwa muda uongezwe kutoka wiki mbili hadi mwezi mmoja kamati ziwe zimekamilika kuundwa.

Wajumbe walishauri wakati wa uundwaji wa mabaraza wajumbe wapate taarifa mapema ili kuweza kufuatilia uundwaji wa mabaraza haya.

**Azimio:**

1. Waumbe waliazimia kazi ya Mabaraza ya Kata ifanyike kwa muda wa wiki mbili hadi tarehe 15 Oktoba, 2018 taarifa iwasilishwe.
2. Wajumbe washiriki katika uanzishwaji wa Kamati na Mabaraza ya Watoto
3. Mashirika yaone uwezekano wa kujenga Hostel kwenye Kata na kujenga Miundombinu mingine ya shule.

**Agenda. Na 4:01:2018/2019: Taarifa ya Wadau Juu ya Ulinzi wa Mtoto (CDF na TAYOA)**

Mwenyekiti alitoa maelezo mafupi kuwa hivi sasa tunao wadau wa CDF na TAYOA ambao wanasaidia juhudi za Halmashauri katika kuhudimia watoto wa Wanawake katika Wilaya yetu.

**Taarifa ya Mradi wa TAYOA**

Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii alitoa taarifa fupi kuhusu mradi wa TAYOA ambao wanafanya kazi kwa kushirikiana na Halmashauri yetu kwa lengo la kudhibiti VVU/ UKIMWI kwa Wasichana Balehe na Wanawake vijana.

Aidha, ufafanuzi ulotolewa kuwa TAYOA wanafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wilayani na kila mdau ana majukumu yake.

Hadi sasa shughuli zilizofanywa na TAYOA wilayani ni kama ifuatavyo:-

1. Usambazaji wa Sanitary Pads (Taulo za Kike)
2. Uhamasishaji kupima VVU na jumla ya watu 2,129 wamepima kutoa elimu ya kujikinga na VVU
3. Kuendesha Bonanza (Kuhamasisha upimaji, Upimaji kansa ya kizazi)
4. Mafunzo kwa waelimisha rika nje ya shule

Wajumbe walishauri kuwa shirika litusaidie tupate vyanzo vya mapato vya kujenga Hostel, tatizo kubwa ni umbali toka nyumbani hadi shuleni hapa ndipo vishawishi vinapatikana na kupata mimba.

Wajumbe pia vijiji vya Chogola Massa tatizo kubwa la mimba linatokana na umbali toka nyumbani hadi shule, pamoja na hostel tatizo ni wazazi hawawapi watoto wao mahitaji muhimu sambamba na hilo elimu itolewe kwa wazazi na watoto.

**Taarifa ya Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF)**

Mratibu wa mradi wa Jukwaa la Utu wa Mtoto alitoa taarifa fupi kuhusu mradi wa CDF ambayo inalenga kujenga uwezo kwa wasichana, kuimarisha mifumo ya ulinzi. Aidha, mratibu alielezea kuwa shughuli za mradi unatekelezwa kwenye Kata za Kibakwe, Pwaga, Belege na Mpwapwa Mjini.

Baadhi ya kazi zilizotekelezwa na Mradi ni kama ifuatavyo:-

- Kuunda vikundi vya malezi
- Mafunzo ya uwezeshaji wa wasichana na kina mama katika ujana balehe kuanzisha shughuli za kiuchumi
- Kujenga uwezo kwa wasichana wa vikundi nje ya shule kwenye Afya ya uzazi, Haki za mtoto na kuhamasisha jamii.
- Kujenga uwezo kwa watendaji, polisi na walimu juu ya Haki na ulinzi wa mtoto
- Kujenga uwezo kamati za Wilaya

- Kujenga uwezo Dawati la Polisi Mpwapwa na Kibakwe
- Kujenga uwezo wa uendeshaji wa Kesi za watoto
- Maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika
- Midahalo ya wasichana na wavulana kuhusu haki za mtoto, afya ya uzazi na ukatili wa kijinsia.
- Uelimishaji jamii juu ya haki za watoto na ukatili wa kijinsia
- Kujenga uwezo wasichana ndani ya shule kupitia Club za CDF.

Aidha, mratibu alielezea baadhi ya Changamoto, athari na Hatua zilizopendekezwa.

Wajumbe kwa pamoja waliipokea taarifa kwa pamoja za TAYOA na CDF na kuzijadili.

Mwenyekiti alishauri kuwa CDF na Tayoa wanafanya shughuli zinazofanana hivyo alishauri kuwa ni vizuri kuwaunganisha pamoja ili tusije kurudia kazi mara mbili sehemu moja. Kama mashirika haya yanafanya kazi kwa pamoja tutafika sehemu kubwa.

Wajumbe walijadili kuwa idadi ya mimba ni kubwa, watu hawa wanajulikana lakini matatizo yamekuwepo kwenye utoaji wa ushahidi Mahakamani. Wajumbe walishauri kuwa sisi kama Kamati tujiulize kuwa tutafanya nini kuhusu mimba za utotoni na Mashuleni, ambapo kesi zikifika Polisi watuhumiwa wanakuwa hawafahamiki.

Wajumbe waliyapongeza mashirika ya CDF na TAYOA kuwa wamefanya kazi nzuri, hivyo kama Kamati kwa kushirikiana na mashirika haya tuwe na kauli ya pamoja ya Wilaya kuwa kila Kata tujenge Hosteli ili Serikali iweke mkazo wake.

Mh. Hakimu alitoa alitoa ushauri kuwa kubwa zaidi elimu kwa wazazi lazima mtoto ajengewe misingi mizuri ya maadili kwa watoto hivyo watoto kama hawana maadili hata wakienda sehemu nyingine atakuwa bado ameharibika kimaadili. Vilevile ni vigumu kutoa hukumu kama hakuna ushahidi wa kutosha uwezi kumfunga mtu ambaye hana hatia. Sheria inasema afadhali kuwaacha huru watu 100 waliokosa kuliko kumfunga mtu mmoja ambaye hajafanya kosa. Cha msingi ni ushirikiano wazazi ndio chanzo cha mmomonyoko wa maadili hivyo elimu itolewe kwa wazazi na jamii. Tusikubali kumaliza kesi kienyeji enyeji, na mihimili iliyokuwepo tushirikiane kwenye ngazi zote.

**AGENDA Na 7/2018/19: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 08:45 mchana kwa kuwashukuru wajumbe kwa usikivu wao na uchangiaji, tumefanya kikao kwa ajili ya Maendeleo ya Wilaya ya Mpwapwa na tumepata Mpango Kazi ambao utakuwa kama dira ya Utekelezaji kwa kipindi cha miezi mitatu. Pia aliwakumbusha wajumbe kuwa kikao kijacho kitafanyika tarehe 06/12/2018.

| | |
|---|---|
| …………………………… | ……………………… |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |